# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuanza hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kufika katika Baraza lako hili leo tukiwa wazima na kuendelea kutekeleza majukumu yetu ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuijenga nchi yetu. Aidha, nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kutoa Maoni ya Kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato
ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kukamilika kwa hotuba hii na kuweza kuiwasilisha katika Baraza lako ni kutokana na mashirikiano makubwa niliyoyapata kutoka kwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bajeti. Aidha, Naishukuru Idara ya Ushauri wa Kisheria ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa miongozo yao mbali mbali katika kuikamilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuendelea kutoa Maoni ya Kamati kuhusiana na Mswada huu napenda kuchukua nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Bajeti na Sekretarieti kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Abass Vuai Moh’d | Katibu |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 9. | Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 10. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

## UCHAMBUZI WA MSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Mswada huu ni kurekebisha baadhi ya kodi na ushuru na kufanya marekebisho ya sheria za fedha na kodi zinazohusiana na makusanyo na usimamizi wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu iliupitia Mswada huu na kuibua marekebisho mbali mbali, baadhi ya marekebisho hayo ya kisarufi ambapo vifungu mbali mbali vimerekebishwa ili kuvifanya visomeke vizuri na vilete maana iliyokusudiwa na marekebisho mengine yanayotokana na makosa ya kiuchapaji ambayo yamerekebishwa ili kuweka bayana usahihi wa maneno hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekubaliana na marekebisho ya Sheria hizo baada ya kufanyika marekebisho iliyopendekeza. Baada ya kikao cha majadiliano na Afisi ya Rais – Fedha na Mipango, Kamati imeridhia marekebisho yote ya sheria zifuatazo:

i. Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, Nam. 7 ya 2009
ii. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998
iii. Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya 2008
iv. Sheria ya Ushuru wa Stempu, Nam. 7 ya 2017
v. Sheria ya Usafiri wa Barabarani, Nam. 7 ya 2003
vi. Sheria ya Mafunzo ya Amali, Nam. 11 ya 2007
vii. Sheria ya Fedha na Usimamizi wa Mapato ya Umma, Nam. 9 ya 2015

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kupata ufafanuzi wa kina wa baadhi ya marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati ya Bajeti, nawaomba Wajumbe wako waupitie waraka wa Kamati wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Mswada huu ambao wamepatiwa.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa ya kuwasilisha hotuba hii ya Maoni ya Kamati ya Bajeti na ni matarajio yangu kwamba, maoni haya ya Kamati niliyoyawasilisha yatasaidia katika kuimarisha mswada huu

na kuweka msingi mzuri wa usimamizi wa sheria za fedha na kodi zilizorekebishwa kupitia mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza hili kwa utulivu wao wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha Maoni haya ya Kamati na nawaomba wauchangie na kuupitisha Mswada huu ili kuzipa fursa taasisi zilizopewa majukumu ya kukusanya na kudhibiti mapato kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

…………………….

Mhe. Abdulla Hussein Kombo,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**